NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

Ridván 2026

Kwa Wabahá’í wa Ulimwengu,

Marafiki wapendwa sana,

Sasa inaanza awamu ya pili, kubwa zaidi ya Mpango wa Miaka Tisa. Tunaiona jumuiya ya Kibahá’í ya ulimwengu ikisonga mbele kwa mshikamano, ikiwa na imani kabisa katika mwelekeo iliojiwekea. Udhahiri na uthabiti wake vipo wazi kabisa. Bila kutishika na ghasia ziongezekazo ulimwenguni, imejikita katika dhima yake takatifu. Tunafurahi hasa kuona waumini waliothibitishwa hivi karibuni wakichukua nafasi yao kwa shauku katika uwanja wa huduma na utendaji sambamba na wale waliothibitishwa muda mrefu katika Imani. Klasta za hatua ya tatu zinathibitisha kuwa ni ardhi yenye rutuba ambapo tajiriba tele zinaweza kuvunwa na kusambazwa. Na tumefurahishwa kuona marafiki kila mahali wakitafakari juu ya ujumbe tuliowaandikia Washauri ambao walikusanyika hapa mwezi Desemba na wakitumia maudhui yake kadiri wanavyopanga na kutenda.

Moyo huu wenye nia hususan umedhihirika zaidi katika mikutano ya kiasasi iliyoitishwa kote ulimwenguni. Mara kwa mara, taarifa za mikutano hii zimeeleza jambo lile lile: mazungumzo ya kina na yenye umaizi, yatokanayo na tajiriba ya moja kwa moja ya kujenga jumuiya hai badala ya dhana au nadharia. Mazungumzo haya yanahuishwa na mchakato endelevu wa ujifunzaji kila mahali. Yamejazwa na utambuzi wa kina zaidi wa umuhimu wa jitihada za jumuiya ya Kibahá’í na matokeo yake kwa ulimwengu wenye misukosuko ulio katika uhitaji mkubwa wa mwongozo. Hisia ya uwajibikaji na azma inaonekana kwa mapana, na kuna ufahamu wa kina wa ukubwa wa kazi iliyo mbele yetu. Mara nyingi, mazungumzo haya hukaribisha mtazamo wa ziada na unaokamilishana ambao hutambua juhudi za jumuiya na watu binafsi siyo tu kama utekelezaji wa programu na miradi, bali pia kama ukuzaji wa mtindo wa maisha unaofuata mafundisho matakatifu—uelekezaji wa matendo, miingiliano na matamanio.

Mazungumzo haya haya yenye ari, yakiakisi kujitoa kwa ajili ya ujifunzaji, yanaendelezwa katika jumuiya nzima kuanzia ngazi ya kitaifa na kanda hadi kijiji na ujirani, na katika mazingira mbalimbali, ikiwemo mikutano iliyoandaliwa na asasi hali kadhalika nafasi zingine zinazoibuka. Kwa hakika yatakuwa ndiyo sura ya Mikutano Mikuu ya Kitaifa vile vile. Tunatarajia kuona ruwaza za hatua za mtu binafsi na za pamoja zikiimarishwa na kupanuliwa kadiri mazungumzo haya yanavyokunjuka. Kama ilivyo ada, ni mazungumzo ndiyo yanayopaswa kupanuliwa hadi kwenye makundi yapanukayo daima ya marafiki, majirani na roho zingine zenye fikra sawa ambazo zinajihusisha na juhudi za kuleta maendeleo ya kiroho na kimwili yatokanayo na umoja wa jamii ya binadamu. Nafasi zinazoundwa kwa ajili ya kupanua mazungumzo haya—ziwe za ghafla au zilizopangwa toka muda mrefu—ni ishara ya ujihusishaji thabiti na jamii, na tunatumai zitakuwa za kawaida zaidi na zaidi.

Wengi wanaokutana na shughuli za mashinani za Wabáhá’í katika jamii pana hushangazwa na sifa zake za kipekee: zinatokana na shauku ya kweli kwa ajili ya ustawi wa wote,

zinalenga kukuza umoja na huduma, na zinafuata kanuni dhahiri na hazidhani kama zina jibu la haraka kwa kila tatizo. Kwa moyo wa jitihada ya pamoja, Wabáhá'í wanatafuta kushirikiana na wengine na kujifunza kwa pamoja; na katika uhusiano wanaouanzisha na wale wanaoshika nafasi za mamlaka na uwajibikaji katika jamii, wao ni wenye ari na mtazamo wa mbali. Wao wanatekeleza mabadiliko ya kijamii pasipo na tamaa ya kisiasa au maslahi binafsi, na wanatambua kwamba, kadiri umaarufu wa Imani unavyoongezeka, inakuwa muhimu kuhakikisha kwamba sifa na shabaha zake halisi zinaeleweka vyema. Katika maeneo mengi, kina kiongezekacho cha miingiliano ya jumuiya na jamii humaanisha, pasipo kuepukika, kwamba kuna hali mpya za kuzishughulikia na maswali mapya ya kujibu, na hili linaichochea jumuiya kukuza zaidi uwezo wake.

Kama tulivyoeleza katika ujumbe wetu kwa Kongamano la hivi karibuni la Washauri, maendeleo makubwa katika miaka minne iliyopita yamekuwa ni uibukaji wa jumuiya kama nguli dhahiri zaidi wa Mpango, ikijipanga ili kukidhi mahitaji maalum na kuendeleza nyanja maalum za jitihada, kutoa msaada wa pamoja kupitia mipangilio shirikishi, na kujifunza kuwa wenye ufanisi zaidi ndani ya muundo ubadilikao wa utendaji. Mfano wa kuvutia wa hili ni makundi ya vijana, yakifanya kazi kwa pamoja katika eneo fulani na kuhamasisha ushiriki wa wenzao. Kwa kawaida, jitihada zao zinanufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na utiaji moyo na miongozo yenye upendo ya asasi, lakini vijana pia wameonesha uwezo wao wa kuthubutu na kubaini fursa za huduma zenye kuzaa matunda. Mara nyingi, jitihada zao hutokea katika mazingira yenye migogoro na machafuko, ukosefu wa usawa wa kiuchumi, na migawanyiko mikubwa ya kijamii. Tunatambua changamoto zinazowakabili vijana katika hali hizo, na tunawapongeza kwa kujiepusha na msukumo wa kukosoa na kulaumu, badala yake wakitafuta njia zinazojenga ili kuepuka vizuizi hivi vikubwa na hatimaye kufanya kazi hadi kuvishinda.

Marafiki wapendwa, licha ya misukosuko ya nyakati hizi, tunawasisitiza msiwe na hofu wala kukata tamaa. 'Abdu'l-Bahá anatushauri sote kutegemea baraka za Mungu, na hivyo kuwa "wenye matumaini daima", kuwa "imara" katika matumaini yetu, na kuwa "chanzo cha matumaini kwa roho zilizokata tamaa". Wakati peo za ulimwengu zinapokuwa gizani, matumaini yanakuwa rasilimali adimu na ya thamani—lakini ile ambayo jumuiya ya Jina Kuu Kabisa imebarikiwa nayo kwa wingi kwa sababu ya imani yake kuhusu mustakabali wa jamii ya binadamu na kwa sababu ya yale iliyojifunza kutokana na tajiriba yake yenyewe. Kaumu hutamani sana matumaini mnayoweza kuleta mioyoni mwao.

Kwa mfano mzuri sana wa jumuiya ambayo imehifadhi kwa muda mrefu mwale wa matumaini, tunawaangalia wafuasi wa Bahá'u'lláh waliodhulumiwa lakini daima wenye subira, daima thabiti, daima wenye uvumilivu katika Chimbuko la Imani Yake. Tazama jinsi walivyobakia wenye nidhamu, jinsi walivyojitoa kwa kanuni licha ya miongo isiyoisha ya ukandamizaji—na jinsi walivyoazimia kujifunza kutokana na maendeleo yaliyofanywa na waumini wenzao katika nchi zingine, jinsi walivyodhamiria kuwatumikia na kuwafariji raia wenzao katika nchi yao wenyewe. Kwa wengi mno wa wananchi wenzao, wamekuwa, na wameendelea kuwa, taa ya matumaini, chanzo cha huruma na umaizi, na wenzi wa kuaminika katika njia ya huduma. Katika wiki na miezi ya hivi karibuni, marafiki hawa tunaowapenda sana daima wamekuwa katika fikra zetu na kiini cha mara kwa mara cha sala zetu, kama tulivyo na hakika wamekuwa hivyo kwenu, tukimuomba Bwana Mwenye Upendo-Daima kuwaweka ndani ya pambaja la uangalizi Wake wenye upendo.

Jitihada zenu wenyewe za kuendeleza Hoja ya Mungu ndiyo shabaha ya sala tunazotoa kwenye Kizingiti Kitakatifu—hususan sasa, katika kuanza kwa awamu mpya ya Mpango wa Miaka Tisa. Tunapoenda mara kwa mara kwenye Makaburi Matakatifu, tunaomba auni na msaada mtakatifu kwa ajili ya jitihada zenu, na tunasihi katika kazi zenu ustahimilivu na nguvu. Muwe wepesi wa kutenda na wenye shauku ya kujifunza, na baraka zote za Ufalme wa Mbinguni na ziwe zenu.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.